Government of Western Australia
Department of Health

# MAELEZO KUHUSU UKINGAJI WA MATITI KUPITIA UCHUNGUZI WA EKSREI

BreastScreen WA
WA's only accredited screening service

## Karibu katika Kliniki ya Ukingaji Wa Matiti hapa Australia ya Magharibi (BreastScreen WA)...

Tafadhali soma habari hii ya muhimu kuhusu ukingaji wa matiti kupitia uchunguzi na ujaze fomu inayoandamana kama idhini yako KABLA ya kufanyiwa uchunguzi wa matiti. Ukiwa na maswali yoyote wafanyi kazi wa sehemu hii wanaweza kukusaidia. Tafadhali kumbuka ya kwamba unaweza kutoendelea na uchunguzi wakati wowote.

### Kuhusu mpango wa uchunguzi wa matiti

Lengo la mpango wa ukingaji wa matiti ni kuzuia vifo kutokana na ugonjwa wa kansa ya matiti. Picha inayochunguza (eksrei ya matiti) ni njia bora zaidi tunayo kwa sasa ya kuzitambua kansa za matiti zikiwa bado ndogo kutambulika kwa kugusa. Vile tu kansa ya matiti inagunduliwa mapema kabla ya kuenea ndivyo pia inazidisha bahati ya matibabu kufaulu.

Mkazo wa mpango wa BreastScreen WA ni ugunduaji mapema wa kansa ya matiti. Mabadiliko yanayotokea kwa eksirei yako ya uchunguzi ambayo hayafikiriwi kuwa dalili ya kansa ya matiti hayandikwi kwa ripoti.

Ushahidi wa matibabu tunao leo unaonyesha kwamba ukingaji niwa muhimu zaidi kwa wanawake wa kati ya umri wa miaka hamsini hadi sitini na tisa (50-74). Fursa yako ya kupata kansa ya matiti inaongezeka na umri. Karibu asili mia sabini (70%) ya kansa za matiti hutokea kwa wanawake waliotimiza miaka hamsini na kuendelea. Kinga kupitia uchunguzi wa mara kwa mara unaweza kupunguza vifo kati ya wanawake kwa asili mia thelathini (30%). Faida za kinga kupitia uchunguzi wa eksrei ni kidogo kwa wanawake wa chini ya miaka hamsini (50).

### Eksrei ya matiti inafanyika vipi?

**Utaulizwa uvue nguo hadi kiunoni na kupewa gauni ya kuvaa. Mwanamke aliye na ujuzi spesheli wa upigaji picha za eksrei atakuchukua eksrei ya kuchunguza.**

Wakati eksrei hii ya kuchunguza matiti inafanyika matiti hubanwa kwa muda wa sekunde chache ili picha safi ikatokea. Hii huenda ikapunguza starehe.

Kawaida picha mbili hupigwa kila titi lakini wakati mwingine picha zaidi zaweza kuhitajika.

### Nani huisoma picha ya eksrei ya matiti?

**Matokeo ya picha yako itategemea waamuzi wa madaktari wawili spesheli (wenye ujuzi wa upigaji picha za eksrei) ambao wana ustadi mwingi wa usomaji wa eksrei za matiti. Picha zote za eksrei ya matiti husomwa kipekee. Wakati mwingine kama wale madaktari wawili spesheli hawakusikilizana kwa maoni yao, daktari wa tatu ataisoma picha ya eksrei ya matiti yako.**

### Jee nikihitaji kurudiliwa eksrei?

Mara chache tu mpigaji picha za eksrei atakuomba arudie eksrei tena kama picha haikutoka safi kutosha. Hii ikihitajika utapokea simu au barua yakukuuliza urudi tena. Hizi eksrei za kurudia zitafanyiwa katika kliniki ya ukingaji.

### Kufahamishwa matokeo

**Wanawake wengi watajulishwa kwa barua kabla ya siku kumi na nne (14) kupita kwamba matokeo yako sawa. Sio jambo lisilo la kawaida wanawake kuitwa ili wafanyiwe uchunguzi au vipimo zaidi. Hii ikihitajika, muuguzi anayeangalia matiti kutoka BreastScreen WA atakuita**

**kwa simu kuzungumzia hayo nawe. Mara nyingi hivi vipimo havitaonyesha shida yoyote itakayosababisha uchunguzi zaidi.**

Wanawake ambao hupimiwa mijini watapangiwa ahadi katika kituo cha upimaji ambapo uchunguzi zaidi wa matiti, au zikihitajika, vipimo zaidi zinaweza kufanyiwa.

Kwa wanawake ambao hupimiwa kwa kituo cha kutembezwa na gari mashambani, vipimo au uchunguzi zaidi wa matiti hufanyiwa kwenye kituo hicho cha kuzungushwa na gari ili kuwarahisishia mambo.

**Tafadhali kumbuka:** BreastScreen WA hubakia na hizi picha za uchunguzi wa matiti ili kuzilinganisha na zingine za siku za baadaye.

**Hii picha ya eksrei ya matiti inaweza kuaminika?**

**Hizi picha za uchunguzi wa matiti zinaweza kuonyesha asili mia tisini (90%) za kansa ya matiti. Kuna kansa zengine ambazo haziwezi kuonekana kupitia hizi picha. Wanawake wachanga ama wale ambao wanapata matibabu ya kuongezea homoni mwilini wanaweza kuwa na mkusanyiko mzito wa seli mwilini kuliko wanawake wa makamo na hii inaweza kufanya utambulishaji wa kansa ukawa mgumu kupitia kwa picha ya eksrei. Hii huenda ikasababisha wanawake wachanga wakahitaji uchunguzi zaidi, hata pia kipimo cha seli za kansa, sababu ya ugumu wa kutambulisha kansa kupitia kwa njia ya eksrei pekee.**

Pia picha ya uchunguzi wa matiti inaweza kutia wasiwasi mwanzoni lakini uchunguzi zaidi unaweza kuonyesha kwamba hapana shida kuu.

Kufanyiwa picha ya uchunguzi wa matiti hakuwezi kuzuilia kansa ya matiti lakini kuitambua kansa mapema inasaidia kuzidisha bahati ya matibabu kufaulu.

**Jee picha ya eksrei ya matiti inaweza kuleta madhara yoyote?**

**Wakati mwingine kubana au kufinywa kwa matiti wakati wa kuchukuliwa picha kunaweza kusababisha titi kuumia au kuchambuka kwa muda mfupi. Hii haisababishi madhara ya baadaye kwa tishu za matiti.**

Kila picha ya uchunguzi hutumia kipimo cha chini zaidi cha mnururisho. Ushahidi wa matibabu tunao leo unaonyesha kwamba kuna hatari ndogo sana inayosababishwa na utumiaji wa mnururisho. Faida za kinga kupitia uchunguzi wa eksrei ya matiti zinapita hii hatari.

Wanawake ambao wanashuku kama huenda wakawa wana mimba wanashauriwa kutofanyiwa hii uchunguzi wa eksrei ya matiti. Kama unadhani kwamba unaweza kuwa na mimba, tafadhali mjulishe ule anaye kukaribisha hapa ama mwenye kuichukua picha ya eksrei.

**Jee kama nina bonge la matiti au shida ya matiti kwa sasa?**

Kama umeona dalili ya bonge katika titi lako, uvujaji wa maji kupitia chuchu la titi ama mabadiliko mengine yoyote ya matiti yako, tafadhali mueleze mwenye kuichukua picha kabla ya kufanyiwa uchunguzi wa eksrei ya matiti. Ni muhimu pia umuone daktari wako kuhusu hizi dalili ingawaje matokeo ya picha ya eksrei yako ya kawaida.

**Mbona niwaambie daktari wangu wa kawaida ni nani?**

Ili uweze kuhudumiwa kwa uangalifu, daktari wako anapashwa kujua habari zote zinazohusu afya na matibabu yako. Tunapendelea kumtumia matokeo ya picha ya uchunguzi wa matiti yako. Kati ya kipindi ambapo unafanyiwa uchunguzi ukisubiria uchunguzi unaofuatia, ni muhimu kukagua matiti yako mara kwa mara na umfahamishe daktari wako mara tu ukiona mabadiliko yoyote. Tungekushauri ukaangaliwa matiti yako na daktari wako mara kwa mara.